# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# TAASISI YA ELIMU TANZANIA

# MUHTASARI WA SOMO LA ELIMU JUMUISHI KWA MWALIMU TARAJALI

# ASTASHAHADA YA UALIMU ELIMU MAALUMU

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2019

Toleo la Kwanza 2019

ISBN: 978-9976-61-841-9

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P. 35094
Dar es Salaam
Tanzania

Simu: +255 222 773 005
Faksi: +255 222 774 420
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Taasisi ya Elimu Tanzania. (2019). Muhtasari wa Somo la Elimu Jumuishi kwa Mwalimu Tarajali Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu. Dar es Salaam: Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kuutoa muhtasari huu kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

## Idhini

Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu ni ya miaka miwili na yamekusudiwa kumuandaa mwalimu tarajali kuwa mahiri na mwenye uwezo wa kufanya kazi kwa dhati na kwa weledi. Mwalimu huyo atafundisha katika shule za msingi zinazodahili wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Mwalimu tarajali atatambuliwa kuwa ni mwalimu baada ya kuhitimu mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu na kufaulu mafunzo ya nadharia na mafunzo ya ualimu kwa vitendo.

Muhtasari huu, umeidhinishwa kuwa ni wa somo la Elimu Jumuishi katika Mtaala wa Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu.



Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kaimu Kamishna wa Elimu
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia
S.L.P. 10
Dodoma

Simu: +255 262 963 533
Baruapepe: info@moe.go.tz
Tovuti: www.moe.go.tz

# YALIYOMO


Idhini ........................................................ iii

1.0 Taarifa za Awali ........................................................ 1

- 1.1 Utangulizi........................................................ 1
- 1.2 Muundo wa Muhtasari ........................................................ 1
- 1.3 Sababu za Kuandaa Muhtasari ........................................................ 2
- 1.4 Malengo ya Elimu Nchini Tanzania........................................................ 2
- 1.5 Malengo ya Jumla ya Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu ........................................................ 3
- 1.6 Madhumuni ya Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu ........................................................ 4
- 1.7 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu........................................................ 4
- 1.8 Malengo ya Somo la Elimu Jumuishi kwa Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu........................................................ 5
- 1.9 Upimaji na Tathmini ........................................................ 6
- 1.10 Muda wa Mafunzo ........................................................ 7
- 1.11 Maudhui ya Muhtasari wa Somo ........................................................ 7

2.0 Maudhui ya Muhtasari........................................................ 8

2.1 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Somo........................................................ 8

2.2 Maudhui ya Ufundishaji wa Somo........................................................ 10

Majedwali

Jedwali namba 1: Upimaji Endelevu na Upimaji Tamati........................................................................... 6

Jedwali namba 2: Umahiri wa Somo la Elimu Jumuishi kwa Mwalimu Tarajali....................................... ... 8

Jedwali namba 3: Maudhui ya Somo la Elimu Jumuishi kwa Mwalimu Tarajali....................................... .... 10

Orodha ya Machapisho ........................................................................................................................ 34

## 1.0 Taarifa za Awali

## 1.1 Utangulizi

Muhtasari huu wa somo la Elimu Jumuishi umeandaliwa kutokana na Mtaala wa Mafunzo ya Ualimu Elimu Maalumu wa mwaka 2019. Muhtasari huu unalenga kumjengea mwalimu tarajali maarifa, stadi na mwelekeo utakaomwezesha kukabiliana na mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji wa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu aliyedahiliwa katika elimu ya msingi.

Ili kumsaidia mkufunzi, yametolewa mapendekezo ya mbinu za kufundishia na kujifunzia, zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia pamoja na upimaji. Mkufunzi anahimizwa kutumia mbinu mbalimbali na zana zinazopatikana kwenye mazingira yanayohusika na upimaji ulioshauriwa kwenye muhtasari huu. Pamoja na mbinu zilizoainishwa kwenye muhtasari huu mkufunzi anaweza kutumia mbinu nyingine tofautitofauti kulingana na mazingira na mahitaji ya mwalimu tarajali na umahiri unaojengwa.

## 1.2 Muundo wa Muhtasari

Muhtasari huu umegawanyika katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ina taarifa za awali na sehemu ya pili ni maudhui ya muhtasari.

Sehemu ya kwanza inajumuisha utangulizi, muundo wa muhtasari, sababu za kuandaa muhtasari, malengo ya elimu nchini Tanzania, malengo ya jumla ya mafunzo ya astashahada ya ualimu elimu maalumu, madhumuni ya mafunzo ya astashahada ya ualimu elimu maalumu, umahiri wa jumla wa mafunzo ya astashahada ya ualimu elimu maalumu, malengo ya somo la Elimu Jumuishi, upimaji na tathmini na muda wa mafunzo. Sehemu ya pili inajumuisha maudhui ya muhtasari wa somo.

## 1.3 Sababu za Kuandaa Muhtasari

Dira ya elimu na mafunzo, inasisitiza kuwapo kwa mwalimu aliye bora kitaaluma na kitaalamu na mwenye mbinu mbalimbali za kufundishia na kujifunzia ili kukabiliana na changamoto za mahitaji na matarajio ya kielimu kulingana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Mwelekeo wa dira na mpango wa elimu kwa ujumla ni kumuandaa mwalimu mwenye ujuzi wa kufundisha masomo kwa mwanafunzi wa shule ya msingi mwenye mahitaji maalumu, kwa kuzingatia misingi, kanuni na mielekeo na mahitaji maalumu ya mwanafunzi. Mkufunzi wa somo la Elimu Jumuishi anatakiwa kumjengea ujuzi mwalimu tarajali ili aweze kuyatumia vema mazingira yake katika kumwezesha mwanafunzi wa elimu ya msingi mwenye mahitaji maalumu kujifunza na kuyamudu mazingira yanayomzunguka kwa kumpatia afua stahiki.

## 1.4 Malengo ya Elimu Nchini Tanzania

Elimu inayotolewa ni ya kurithisha maarifa, stadi na mielekeo bora kutoka kwa vizazi vilivyopita hadi vizazi vya wakati huu na vijavyo. Hivyo, yafuatayo ndiyo malengo makuu ya elimu nchini:

a) kuendeleza na kukuza maendeleo, kuboresha haiba ya wananchi wa Tanzania, rasilimali zao na matumizi bora ya rasilimali hizo katika kuleta maendeleo ya mtu binafsi na ya kitaifa;

b) kukuza tabia ya kuthamini utamaduni, mila na desturi za watanzania;

c) kukuza upatikanaji wa fursa za kusoma, kuandika na kuhesabu na matumizi sahihi ya maarifa na stadi za kijamii, kisayansi, kiufundi, kiteknolojia, kitaalamu na aina nyingine za maarifa na ujuzi, kwa ajili ya maendeleo na kuboresha hali ya mtu na jamii;

d) kukuza na kuendeleza kujiamini, kudadisi, weledi na kuheshimu utu wa mtu na haki za binadamu na kuwa tayari kufanya kazi kwa kujiendeleza na kwa maendeleo ya Taifa;

e) kuwezesha na kupanua mawanda ya kujipatia maarifa, kuboresha na kukuza stadi za kiakili, utendaji, uzalishaji na nyingine zinazotakiwa katika kukidhi mabadiliko ya mahitaji kiuchumi;

f) kumwezesha kila raia kuelewa misingi ya katiba ya nchi pamoja na kuthamini haki za binadamu na uraia, wajibu na majukumu yanayoendana nayo;
g) kukuza utashi wa kupenda na kuheshimu kazi za kujiajiri na kuajiriwa na kuboresha utendaji kazi katika sekta za uzalishaji na huduma;
h) kujenga misingi ya maadili yanayokubalika kitaifa na ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na sheria kwa njia ya kujifunza;
i) kuwezesha kuwapo kwa matumizi sahihi, usimamizi na utunzaji wa mazingira; na
j) kujenga tabia na utamaduni wa kuwakubali watu wenye ulemavu na kuwashirikisha kwenye nyanja zote za maisha kwa maendeleo ya Taifa.

## 1.5 Malengo ya Jumla ya Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu

Mafunzo ya Ualimu Elimu Maalumu yana malengo yafuatayo:

a) kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika nadharia za saikolojia ya elimu, malezi, ushauri na huduma kwa watu wenye ulemavu;
b) kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika kugundua na kubuni mbinu na njia za kufundishia na kujifunzia;
c) kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika uchambuzi wa mtaala na vifaa vya mtaala;
d) kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika kumudu stadi kuu za masomo ya lugha, sanaa na maendeleo ya sayansi na teknolojia;
e) kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika kufanya upimaji na tathmini ya maendeleo katika elimu;
f) kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika stadi za uongozi na utawala katika elimu; na
g) kujenga umahiri wa mwalimu tarajali katika kumfundisha mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu.

## 1.6 Madhumuni ya Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu

Mwishoni mwa mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu ya muda wa miaka miwili, mwalimu tarajali aweze:

a) kutafsiri mtaala wa elimu ya msingi na mihtasari yake katika masomo darasani;
b) kuandaa na kutumia njia shirikishi katika ufundishaji/ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi;
c) kubuni, kuendeleza na kufaragua zana za ufundishaji na ujifunzaji katika elimu ya msingi kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi;
d) kufanya tafiti tatuzi za kielimu ili kuwabaini, kuwaendeleza na kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika shule za msingi;
e) kurithisha desturi, maadili na tabia zinazokubalika kwa wanafunzi wa shule za msingi;
f) kuchagua, kupanga, kusimamia na kuongoza vipindi darasani katika shule za msingi;
g) kufundisha kwa ufanisi masuala mtambuka; na
h) kutunga na kusahihisha majaribio na mitihani inayoendana na mtaala wa elimu ya msingi kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi katika nyanja zote tatu za kujifunza.

## 1.7 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu

Umahiri mkuu wa mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu umejikita katika kumuandaa mwalimu tarajali aweze:

a) kumbaini mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu, kujenga misingi ya kukubalika kwa wenzake, kwa jamii na kumpatia afua stahiki;
b) kutumia mazingira wezeshi ya ufundishaji na ujifunzaji kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu;
c) kutumia njia mbalimbali za mawasiliano na teknolojia saidizi kwa kuzingatia mahitaji maalumu ya mwanafunzi;
d) kutumia mbinu mbalimbali katika kutambua vipaji walivyonavyo wanafunzi wenye mahitaji maalumu na namna ya kuviendeleza;

e) kufanya tafiti tatuzi za kielimu ili kuwabaini na kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika shule za msingi;
f) kutumia misingi na stadi za uongozi katika kuongoza taasisi mbalimbali za elimu;
g) kutumia, kutunza na kukarabati vifaa saidizi vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu;
h) kutumia sanaa na michezo rekebifu katika kuibua na kuendeleza vipaji mbalimbali vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu;
i) kutumia misingi ya ufundishaji na ujifunzaji kufundishia masomo ya taaluma;
j) kujenga umahiri wa masomo kwa mwalimu tarajali utakaomwezesha kuelewa masomo vema na hivyo kumfundisha mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu; na
k) kushirikiana na familia za wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika kuwajengea wanafunzi hao kujiamini, tabia ya kujifunza na kukuza vipaji walivyonavyo.

## 1.8 Malengo ya Somo la Elimu Jumuishi kwa Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu

Muhtasari wa somo la Elimu Jumuishi umeandaliwa ili kumwezesha mwalimu tarajali kufikia malengo yafuatayo:

a) kudumisha elimu jumuishi iliyo bora, inayozingatia usawa na kutoa fursa za ujifunzaji endelevu kwa watu wote;
b) kuimarisha mbinu za kuwawezesha watoto wenye mahitaji maalumu kumudu masomo mbalimbali;
c) kukuza uelewa wa elimu maalumu katika jamii ya shule na kuondoa dhana potofu dhidi ya watoto wenye mahitaji maalumu;
d) kukuza stadi za kiuongozi na kiutawala katika utekelezaji wa elimu jumuishi;
e) kutumia mbinu za ufundishaji na ujifunzaji katika kutengeneza na kufaragua zana jumuishi;
f) kutekeleza misingi ya elimu jumuishi katika elimu ya msingi;
g) kutumia mbinu jumuishi katika kufanya upimaji wa kielimu; na
h) kutatua changamoto za elimu jumuishi katika ngazi ya shule ya msingi.

## 1.9 Upimaji na Tathmini

Muhtasari huu umependekeza mbinu mbalimbali za upimaji na tathmini kwa kuzingatia mahitaji ya mwalimu tarajali wakati wa mchakato wa ujifunzaji wa somo la Elimu Jumuishi. Upimaji tamati utafanywa na Baraza la Mitihani la Tanzania na utakuwa na alama 50. Upimaji endelevu utafanywa na mkufunzi wakati mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji unaendelea na utakuwa na alama 50. Upimaji huu unahusisha majaribio, kazimradi, kazi binafsi, mkoba wa kazi, kazi kwa vitendo na mitihani ya mwisho wa mihula. Uzito wa kila aina ya upimaji umeoneshwa katika jedwali lifuatalo:

Jedwali namba 1: Upimaji Endelevu na Upimaji Tamati

| **Vipengele** | **Njia za Upimaji** | **Mwaka** | | | | **Idadi** | **Alama %** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Mwaka wa I** | | **Mwaka wa II** | | | |
| | | **Muhula wa I** | **Muhula wa II** | **Muhula wa I** | **Muhula wa II** | | |
| Taaluma | Majaribio | 2 | 2 | 2 | 2 | 8 | 10 |
| | Kazimradi | 1 | | 1 | | 2 | 5 |
| | Kazi binafsi | 2 | 2 | 2 | | 6 | 5 |
| | Kazi kwa vitendo | 1 | 1 | 1 | | 3 | 5 |
| | Mkoba wa kazi | 1 | | 1 | | 2 | 5 |
| | Mtihani wa mwisho wa muhula | 1 | 1 | 1 | | 3 | 20 |
| Upimaji endelevu | | | | | | | 50 |
| Upimaji tamati: Mtihani wa Baraza la Mitihani la Tanzania | | | | | 1 | 1 | 50 |
| **Jumla ya alama za upimaji endelevu na upimaji tamati** | | | | | | | **100** |

## 1.10 Muda wa Mafunzo

Muhtasari huu wa somo la Elimu Jumuishi katika mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu, umekusudiwa kukamilishwa kwa kipindi cha miaka miwili. Mtazamo wa somo hili ni kumjengea mwalimu tarajali misingi muhimu ya kumwezesha kuimarisha utoaji wa Elimu Jumuishi katika jamii. Masuala mtambuko ya kielimu na ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu yamezingatiwa katika maudhui.

## 1.11 Maudhui ya Muhtasari

Maudhui ya muhtasari yamepangwa katika jedwali yakihusisha umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za kutendwa na mwalimu tarajali, vigezo vya upimaji, viwango vya utendaji na idadi ya vipindi.

### 1.11.1 Umahiri

Ni uwezo wa kufikiri na kutenda kwa ufanisi.

### 1.11.2 Umahiri Mkuu

Ni uwezo wa kutenda jambo kwa ufanisi unaokusudiwa kufikiwa na mwalimu tarajali baada ya kujifunza kwa muda fulani. Umahiri mkuu hujengwa na umahiri mahususi kadhaa atakaojenga mwalimu tarajali kwa kutenda shughuli mbalimbali.

### 1.11.3 Umahiri Mahususi

Ni uwezo atakaojengewa mwalimu tarajali katika kutenda shughuli mbalimbali kwa muda maalumu.

### 1.11.4 Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali

Ni vitendo ambavyo mwalimu tarajali anapaswa kuvifanya ili kufikia umahiri mahususi uliokusudiwa.

#### 1.11.5 Vigezo vya Upimaji

Ni viwango vya ufanisi wa utendaji wa mwalimu tarajali ili kufikia umahiri mahususi.

#### 1.11.6 Viwango vya Utendaji

Ni kiasi cha ufikiwaji wa vigezo vya kila shughuli anayotenda mwalimu tarajali.

#### 1.11.7 Idadi ya Vipindi

Idadi ya vipindi ni makadirio ya muda utakaotumika katika kufundisha na kujifunza kwa kuzingatia uzito wa umahiri na shughuli za kutendwa na mwalimu tarajali. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika 60. Somo hili litafundishwa kwa vipindi viwili kwa wiki. Hata hivyo, mapendekezo haya ya idadi ya vipindi yanaweza kubadilika kulingana na mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

## 2.0 Maudhui ya Muhtasari

### 2.1 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Somo

Jedwali namba 2: Umahiri wa Somo la Elimu Jumuishi kwa Mwalimu Tarajali

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|
| 1.0 Kukuza matumizi ya elimu jumuishi nchini Tanzania | 1.1 Kufafanua dhana ya elimu jumuishi<br>1.2 Kueleza historia ya elimu jumuishi kitaifa na kimataifa<br>1.3 Kuchambua mikakati ya kitaifa inayokuza elimu jumuishi |
| 2.0 Kutumia misingi ya elimu jumuishi kutatua changamoto za mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu | 2.1 Kueleza nadharia kuhusu ulemavu<br>2.2 Kuchambua mitazamo na changamoto za elimu jumuishi<br>2.3 Kuunda darasa jumuishi |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|
| 3.0 Kutumia mikakati ya elimu jumuishi kutoa elimu bora na afua stahiki | 3.1 Kutumia mbinu za kufundishia katika darasa jumuishi<br>3.2 Kutumia zana jumuishi katika ufundishaji na ujifunzaji<br>3.3 Kufanya upimaji katika elimu jumuishi<br>3.4 Kutoa afua stahiki kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu |
| 4.0 Kutumia mfumo stahiki wa uongozi na usimamizi katika kutekeleza elimu jumuishi | 4.1 Kufafanua dhana ya uongozi na usimamizi katika elimu jumuishi<br>4.2 Kuchambua mfumo wa uongozi na usimamizi wa elimu jumuishi nchini Tanzania<br>4.3 Kutumia mpango jumuishi wa jumla wa maendeleo ya shule |

## 2.2 Maudhui ya Ufundishaji wa Somo

Jedwali namba 3: Maudhui ya Somo la Elimu Jumuishi kwa Mwalimu Tarajali

<table>
<tr><th rowspan="2">Umahiri Mkuu</th><th rowspan="2">Umahiri Mahususi</th><th rowspan="2">Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali</th><th rowspan="2">Vigezo vya Upimaji</th><th colspan="4">Upimaji wa Viwango vya Utendaji</th><th rowspan="2">Idadi ya vipindi</th></tr>
<tr><th>Utendaji Chini ya Wastani</th><th>Utendaji wa Wastani</th><th>Utendaji Mzuri</th><th>Utendaji Mzuri Sana</th></tr>
<tr><td rowspan="3">1.0 Kukuza matumizi ya elimu jumuishi nchini Tanzania</td><td rowspan="3">1.1 Kufafanua dhana ya elimu jumuishi</td><td>a) Kueleza dhana ya elimu na umuhimu wa elimu</td><td>Dhana na umuhimu wa elimu imeelezewa kwa kutoa mifano.</td><td>Anaelezea dhana ya elimu kwa kuzingatia maana.</td><td>Anaelezea dhana ya elimu kwa kuzingatia maana na umuhimu.</td><td>Anaelezea dhana ya elimu kwa kuzingatia maana, umuhimu na kutoa mifano.</td><td>Anaelezea dhana ya elimu kwa kuzingatia maana, aina na umuhimu na kutoa mifano kulingana na mazingira .</td><td rowspan="3">8</td></tr>
<tr><td>b) Kueleza dhana ya ujumuishi</td><td>Dhana ya ujumuishi imeelezewa kwa kutoa mifano.</td><td>Anaelezea dhana ya ujumuishi kwa kuzingatia maana.</td><td>Anaeleza dhana ya ujumuishi na kutaja viashiria vya ujumuishi kwa kuzingatia maana.</td><td>Anaeleza dhana ya ujumuishi kwa kuzingatia maana na aina.</td><td>Anaeleza dhana ya ujumuishi kwa kuzingatia maana, aina, viashiria na kutoa mifano.</td></tr>
<tr><td>c) Kueleza dhana ya elimu jumuishi</td><td>Dhana ya elimu jumuishi imeelezwa kwa kuzingatia vigezo vitatu.</td><td>Anaeleza maana ya elimu jumuishi kwa kuonesha viashiria kwa kuzingatia kigezo kimoja.</td><td>Anaeleza maana ya utoaji wa elimu jumuishi kwa kuonesha viashiria kwa kuzingatia vigezo viwili.</td><td>Anaeleza maana na umuhimu wa elimu jumuishi kwa kuonesha viashiria kwa kuzingatia vigezo vitatu.</td><td>Anaeleza maana na umuhimu wa elimu jumuishi kwa kuonesha viashiria kwa kuzingatia vigezo vitatu na kutoa mifano.</td></tr>
</table>

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji Chini ya Wastani | Utendaji wa Wastani | Utendaji Mzuri | Utendaji Mzuri Sana | |
| | | d) Kutofautisha elimu jumuishi na mifumo mingine ya utoaji wa elimu | Elimu jumuishi inatofautishwa na mifumo mingine mitatu ya utoaji wa elimu kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu. | Anatofautisha elimu jumuishi na mfumo mwingine mmoja wa utoaji wa elimu kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu. | Anatofautisha elimu jumuishi na mifumo mingine miwili ya utoaji wa elimu kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu. | Anatofautisha elimu jumuishi na mifumo mingine mitatu ya utoaji wa elimu kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu. | Anatofautisha elimu jumuishi na mifumo mingine mitatu ya utoaji wa elimu kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu kwa kutoa mifano. | |
| | | e) Kueleza umuhimu wa elimu jumuishi | Umuhimu wa elimu jumuishi umeelezewa kwa kutumia hoja nne na mifano kulingana na mazingira. | Anaelezea umuhimu wa elimu jumuishi kwa kutoa hoja moja. | Anaelezea umuhimu wa elimu jumuishi kwa kutoa hoja mbili. | Anaelezea umuhimu wa elimu jumuishi kwa kutoa hoja tatu. | Anaelezea umuhimu wa elimu jumuishi kwa kutoa hoja nne na mifano kulingana na mazingira. | |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji Chini ya Wastani | Utendaji wa Wastani | Utendaji Mzuri | Utendaji Mzuri Sana | |
| | 1.2 Kueleza historia ya elimu jumuishi kitaifa na kimataifa | a) Kueleza chimbuko la elimu jumuishi | Chimbuko la elimu jumuishi linaelezwa kwa kutumia vigezo vinne na kutoa mifano. | Anaeleza chimbuko la elimu jumuishi. | Anaeleza chimbuko la elimu jumuishi na uanzishwaji wa shule jumuishi. | Anaeleza chimbuko la elimu jumuishi, uanzishwaji wa shule jumuishi na kuelezea changamoto zake. | Anaelezea chimbuko la elimu jumuishi, uanzishwaji wa shule jumuishi, changamoto na wadau wa elimu jumuishi kwa kutoa mifano. | 8 |
| | | b) Kuelezea historia ya elimu jumuishi nchini Tanzania | Historia ya elimu jumuishi nchini Tanzania imeelezewa kwa kutumia hoja nne na mifano kulingana na mazingira. | Anaelezea historia ya elimu jumuishi nchini Tanzania kwa kutoa hoja moja. | Anaelezea historia ya elimu jumuishi nchini Tanzania kwa kutoa hoja mbili. | Anaelezea historia ya elimu jumuishi nchini Tanzania kwa kutoa hoja tatu na mifano. | Anaelezea historia ya elimu jumuishi nchini Tanzania kwa kutoa angalau hoja nne na kutoa mifano kulingana na mazingira. | |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji Chini ya Wastani | Utendaji wa Wastani | Utendaji Mzuri | Utendaji Mzuri Sana | |
| | | c) Kufafanua hatua za maendeleo ya elimu jumuishi | Hatua za maendeleo ya elimu jumuishi zimefafanuliwa kwa kutoa hoja nne na kutoa mifano. | Anafafanua hatua za maendeleo ya elimu jumuishi kwa kutoa hoja moja. | Anafafanua hatua za maendeleo ya elimu jumuishi kwa kutoa hoja mbili. | Anafafanua hatua za maendeleo ya elimu jumuishi kwa kutoa hoja tatu na mifano. | Anafafanua hatua za maendeleo ya elimu jumuishi kwa kutoa hoja nne na kutoa mifano. | |
| | 1.3 Kuchambua mikakati ya kitaifa inayokuza elimu jumuishi | a) Kueleza dhana ya mkakati | Dhana ya mkakati imeelezwa kwa kutoa mifano halisi. | Anaeleza maana ya mkakati. | Anaeleza maana na sifa za mkakati. | Anaeleza maana na sifa za mkakati kwa kulinganisha na hali halisi na kutoa mifano. | Anaeleza maana, sifa na umuhimu wa mkakati na kutoa mifano kwa kulinganisha na hali halisi. | 8 |
| | | b) Kubainisha mikakati ya kitaifa inayokuza elimu jumuishi | Mikakati minne ya kitaifa inayokuza elimu jumuishi imebainishwa kwa kutoa mifano kulingana na hali halisi. | Anabainisha mkakati mmoja wa kukuza elimu jumuishi. | Anabainisha mikakati miwili inayokuza elimu jumuishi. | Anabainisha mikakati mitatu inayokuza elimu jumuishi kwa kutoa mifano. | Anabainisha mikakati minne inayokuza elimu jumuishi kwa kutoa mifano, kulingana na hali halisi. | |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji Chini ya Wastani | Utendaji wa Wastani | Utendaji Mzuri | Utendaji Mzuri Sana | |
| | | c) Kubaini changamoto katika kutekeleza mikakati ya elimu jumuishi | Changamoto nne katika kutekeleza mikakati ya elimu jumuishi zimebainishwa kwa kutoa mifano na kuhusianisha na mazingira halisi. | Anabainisha changamoto moja katika kutekeleza mikakati ya elimu jumuishi. | Anabainisha changamoto mbili katika kutekeleza mikakati ya elimu jumuishi. | Anabainisha changamoto tatu katika kutekeleza mikakati ya elimu jumuishi na kutoa mifano. | Anabainisha changamoto nne katika kutekeleza mikakati ya elimu jumuishi na kutoa mifano akihusianisha mazingira. | |
| | | d) Kubaini mbinu za kutekeleza mikakati ya elimu jumuishi | Mbinu nne za kutekeleza mikakati ya elimu jumuishi zimebainishwa kwa kutoa mifano kuhusianisha na mazingira halisi. | Anabainisha mbinu moja katika kutekeleza mikakati ya elimu jumuishi. | Anabainisha mbinu mbili katika kutekeleza mikakati ya elimu jumuishi. | Anabainisha mbinu tatu katika kutekeleza mikakati ya elimu jumuishi na kutoa mifano. | Anabainisha mbinu nne katika kutekeleza mikakati ya elimu jumuishi kwa kutoa mifano na kuhusianisha mazingira. | |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji Chini ya Wastani | Utendaji wa Wastani | Utendaji Mzuri | Utendaji Mzuri Sana | |
| 2.0 Kutumia misingi ya elimu jumuishi kutatua changamoto za wanafunzi wenye mahitaji maalumu | 2.1 Kueleza nadharia kuhusu ulemavu | a) Kueleza dhana ya ulemavu | Dhana ya ulemavu imeelezwa kwa kutumia aina nne za ulemavu na mifano kulingana na mazingira. | Anaeleza maana na aina moja ya ulemavu. | Anaeleza maana na aina mbili za ulemavu. | Anaeleza maana na aina tatu za ulemavu kwa kutoa mifano. | Anaeleza maana na aina nne za ulemavu kwa kutoa mifano kulingana na mazingira. | 8 |
| | | b) Kueleza dhana ya mahitaji maalumu katika ujifunzaji | Dhana ya mahitaji maalumu katika ujifunzaji imeelezwa kwa kuzingatia istilahi muhimu. | Anaeleza maana ya mahitaji maalumu. | Anaeleza maana ya mahitaji maalumu katika ujifunzaji. | Anaeleza maana na aina za mahitaji maalumu katika ujifunzaji na kutoa maana. | Anaeleza maana, aina za mahitaji maalumu na umuhimu wa mahitaji maalumu kwa kutoa mifano. | |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji Chini ya Wastani | Utendaji wa Wastani | Utendaji Mzuri | Utendaji Mzuri Sana | |
| | | c) Kubainisha mitazamo dhidi ulemavu | Mitazamo mitano kuhusu ulemavu imebainishwa na kutoa mifano. | Anabainisha mitazamo miwili kuhusu ulemavu. | Anabainisha mitazamo mitatu kuhusu ulemavu na kutoa mifano. | Anabainisha mitazamo minne kuhusu ulemavu na kutoa mifano. | Anabainisha mitazamo mitano kuhusu ulemavu na kutoa mifano. | |
| | | d) Kufafanua mahitaji ya ujifunzaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu | Mahitaji ya ujifunzaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu yamefafanuliwa kwa kutoa mifano kulingana na mazingira. | Anafafanua mahitaji ya ujifunzaji kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu kwenye makundi mawili ya ulemavu. | Anafafanua mahitaji ya ujifunzaji kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu kwenye makundi matatu ya ulemavu. | Anafafanua mahitaji ya ujifunzaji kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu kwenye makundi manne ya ulemavu. | Anafafanua mahitaji ya ujifunzaji kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu kwenye makundi matano ya ulemavu na kutoa mifano kulingana na mazingira. | |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji | | | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji Chini ya Wastani | Utendaji wa Wastani | Utendaji Mzuri | Utendaji Mzuri Sana | |
| | 2.2 Kuchambua mitazamo na changamoto za elimu jumuishi | a) Kubaini viashiria vya elimu jumuishi | Viashiria vitano vya elimu jumuishi vimebainishwa kwa kutoa mifano kulingana na mahitaji ya mwanafunzi. | Anabainisha kiashiria kimoja cha elimu jumuishi. | Anabainisha viashiria viwili vya elimu jumuishi. | Anabainisha viashiria vitatu vya elimu jumuishi na kutoa mifano. | Anabainisha viashiria vitano vya elimu jumuishi na kutoa mifano kulingana na mahitaji ya wanafunzi. | 8 |
| | | b) Kubaini mitazamo chanya kuhusu elimu jumuishi | Mitazamo chanya mitano kuhusu elimu jumuishi imebainishwa kwa kutoa mifano. | Anabainisha mtazamo mmoja kuhusu elimu jumuishi. | Anabainisha mitazamo chanya miwili kuhusu elimu jumuishi na kutoa mifano. | Anabainisha mitazamo chanya mitatu kuhusu elimu jumuishi na kutoa mifano. | Anabainisha mitazamo chanya mitano kuhusu elimu jumuishi na kutoa mifano. | |
